GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. **245** R/Akhir-Ju/D/Awwal **1446** AH Novemba– **2024** Nubuwwat **1403** HS BEI TSH 800/=

KILELE CHA TAMASHA LA MICHEZO JAMIA AHMADYYA 2024



Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kilele cha tamasha la siku za michezo katika chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya mwaka huu (2024) kilifanyika siku za jumanne,jumatano na tarehe 8-10 Oktoba 2024 kwa mafanikio makubwa.Mgeni rasmi katika shughuli hizo alikuwa ni Maulana sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad Sahib Amir na mbashiri mkuu hapa nchini. Hafla ya ufunguzi ilifanyika siku ya jumanne ya tarehe 8 Oktoba 2024 majira ya saa 2 kamili asubuhi kwa usomaji wa Kurani Tukufu iliyosomwa na Shadad Said na kufuatiwa na hotuba fupi iliyotolewa na Sheikh Abdul Nasir Bajwa sahib na kisha ilifuata hotuba ya mgeni rasmi. Katika hotuba yake, Mheshimiwa mgeni rasimi alinukuu sehemu ya aya kutoka katika Sura tul Baqara aya ya 248 kisha akasema kigezo kikubwa kinachotakiwa katika jukumu la ubashiri ni elimu na mwili imara na hii ndiyo hali waliyokuwa nayo manabii wa Mwenyezi Mungu.

Hivyo aliwataka wanafunzi kutumia fursa hii kwa ajili ya kuimarisha afya zao ili wawe waalimu bora na wenye afya madhubuti. Baada ya hotuba hiyo ya ufunguzi kutoka kwa Amir Sahib, michezo ikaanza. Kulikuwa na michezo ya kitimu na mengine ya mtu mmoja mmoja. Mashindano ya kitimu ni kama

UK. 03

WAHITIMU WA DARASA LA SABA WAPEWA VYETI

Wanafunzi waliofanya mitihani yao ya kumaliza elimu ya msingi katika shule ya Ahmadiyya Morogoro walipata bahati ya kutunukiwa vyeti. Hafla ya kuwapatia vyeti vijana hao ilifanyika siku ya Alhamisi ya tarehe 10 Oktoba 2024, katika ukumbi wa chuo cha Jamia Ahmadiyya uliopo kihonda Morogoro. Mgeni rasmi katika kikao hicho alikuwa ni maulana sheikh Khawajah muzaffar ahmad sahib Amir na mbashiri mkuu hapa nchini.



Hapo awali mwalimu mkuu wa shule hiyo Bwana Said Kitata alisoma ripoti fupi ya shule ikionyesha maendeleo ya ustawi wa shule. Jumla ya wanafunzi waliohitimu mwaka [2024] ni 23 na hii ni awamu ya 4 yaani mahafali ya 4 na kufanya jumla ya wahitimu kufikia 93.

Mgeni rasmi alipongeza vijana hao kwa kumaliza salama elimu yao ya msingi, naye maulana Abid Mahmood Bhatti sahib Principal Jamia Ahmadiyya na naibu Amir hapa nchini, alipongeza wahitimu hao na kuwakumbusha kuwa kuhitimu elimu ya msingi siyo mwisho wa masomo, hivyo wajiandae vizuri zaidi na hatua inayofuata yaani masomo ya Sekondari, aliwataka wakafanye vizuri ili kuitangaza vyema shule yetu ya Ahmadiyya.

Pia aliwataka wakaendelee kushika kikamilifu maadili mema ili wakawe raia wema popote watakapokuwa.

SHEIKH MUHAMMAD MUNAWAR SAHIB NA USHAURI WA MWANA ALIYEAHIDIWA[ra] >UK .04

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SIASA ZA TANZANIA: SALA NA FUNGA

Ukichunguza kwa makini siasa za Tanzania kabla na baada ya uhuru utagundua kuwa kwa mapana na marefu zimejikita katika maombi, dua, kumkumbuka Mwenyezi Mungu aweze kurahisisha harakati zao za kurejesha haki yao iliyoporwa na mkoloni. Haki ya kuamua mambo yao wenyewe na kujitawala. Kuhusu hili Sheikh Kaluta Amri Abedi analisema hilo katika utenzi wake 'Tanganyika mpya' tukaomba dua baadhi yetu na akazichukua muumba wetu.

Mikutano ya chama cha ukombozi iwe ya ndani au ya nje hadharani ilianza kwa maombi. Viongozi wa dini walipewa kipaumbele kufungua mikutano ya hadhara.


Mkutano mkuu wa TANU uliofanyika Tabora 1958 na kubadilisha kabisa ramani za siasa za nchi hii, ilihusu iwapo chama hicho kushiriki katika uchaguzi wa kura tatu au la' Baada ya kikao kikao ulifanyika mkutano mkubwa wa hadhara mjini Tabora uliohutubiwa na viongozi wengi akiwemo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mwalimu katika hotuba yake alieleza kuwa kutawaliwa ni fedheha na hakuna mtu aliye bora kumtawala mwingine. Alisema wananchi wangetumia njia zote za kistaarabu za kudai haki yao ya kuzaliwa na kama mwingereza angelileta visingizio vya uongo na kweli, wananchi wangepeleka kilio chao kwa Mwenyezi Mungu. Ni katika mkutano huo wananchi walipobubujikwa na machozi na machozi ya yule anayeonewa yana uzito mkubwa mbele ya Allah.

Siku ya uhuru tarehe 09/12/1961 usiku wa manane bendera union jack ya Mwingereza ilipokuwa inashushwa na ya taifa inapandishwa kwenye uwanja wa taifa. Walikuwepo viongozi wawili wa dini Sheikh Mubarak Ahmad akiwakilisha waislamu na Kardinari Laurean Rugambwa akiwakilisha wakristo. Viongozi hawa waliiombea nchi ipate amani na ustawi. Wakati huo huo wimbo wa taifa uliimbwa na wimbo huu si kingine isipokuwa maombi mwanzo hadi mwisho. Vijana wetu wanaimba kila asubuhi kabla ya kuingia darasani. Bunge letu linafunguliwa na kufungwa kwa dua. Utamaduni huu unaweza kueleza siri ya hali ya utulivu na amani ambayo Allah ameendelea kutujalia nayo.

Silaha nyingine iliyotumiwa na chama cha ukombozi ni funga. Ikumbukwe kuwa funga ni ibada ya zamani sana hata kabla ya kuja kwa Islam. Mwalimu Nyerere ameeleza saumu yake ya Bagamoyo, hiyo ilikuwa desturi ya kawaida ya kudai haki ya kujitawala. Mwalimu Nyerere alishitakiwa na serikali ya kikoloni kwa madai ya kuandika maneno ya uchochezi na kuwakashifu ma DC wa kikoloni. Ni kesi iliyovuta hisia kali na wananchi walikuwa na tayari ikiwa chama kingewaamuru chochote na wangeliweza kutimiza matakwa hayo. Baadhi ya wananchi wa TANU walifunga ili Allah Aepushe kikombe hicho cha Kiongozi wao kufungwa.

Silaha hizi mbili za Sala na funga zilituvusha salama katika safari ya kuelekea nchi yenye uhuru na haki na bado tunaweza kutumia silaha hizi mbili kutupeleka kwa jamii iliyojengwa kwenye misingi ya uhuru, usawa, haki na uadilifu. Na la muhimu kabisa mwaka huu 2024 na 2025 Allah Akipenda tutakuwa na uchaguzi wa kuwachagua viongozi wetu. Historia haioneshi picha nzuri wakati nchi za kiafrika zinapoingia katika uchaguzi na hata wakubwa nao wamekumbwa na maradhi hayo.

Tunatoa wito kwa wazalendo wa nchi hii wakumbuke silaha hizo mbili ili chaguzi zetu mbili zituletee umoja na ustawi na ili tuendelee kujenga taifa letu tukiwa tumeweka kila kitu chetu katika mikono ya



QUR'AN TUKUFU

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ﴿٧﴾

8. Na (kumbukeni) Alipotangaza Mola wenu: Kama mkishukuru, bila shaka Nitawazidishieni, na kama mkikufuru, (jueni) hakika adhabu Yangu ni kali sana. ***Sura Ibrahim 14, aya 8***



NUKUU YA HADITHI

عَنْ مُعَاذٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : أَخَذَ بِيَدِهِ وَقَالَ : يَا مُعَاذُ وَاللَّهِ إِنِّي لَأُحِبُّكَ ثُمَّ أُوْصِيكَ يَا مُعَاذُ لَا تَدَعَنَّ فِي دُبُرِ كُلِّ صَلَوٰةٍ تَقُوْلُ : اللَّهُمَّ أَعِنِّي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسنِ عِبَادَتِكَ.
(ابو داؤد كتاب الصلوة باب في الاستغفار)

Imesimuliwa na Hadhrat Mu›adh r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alimshika mkono wake na akasema: Ewe Mu›adh, usiache kusema mara baada ya kila sala maneno haya: Ewe Mola wangu, Nisaidie niweze kukukumbuka na kukushukuru na kukuabudu kwa njia bora sana.



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Katika kitabu chake "Hekima ya Mafundisho ya Islam", Hazrat Mirza Ghulam Ahmad anaandika: "Subira sio kujiuzulu tu kwa bahati mbaya; ni ubora wa juu wa maadili ya uthabiti katika kukabiliana na matatizo na majaribu yote, kuweka moyo imara na kumtegemea Mungu kabisa. Ni kupitia subira ndipo mtu anapata ukaribu na Mwenyezi Mungu na maendeleo ya kiroho."- (Hekima ya Mafundisho yaUislamu)

Vyanzo hivi vinasisitiza thamani ya subira katika imani na kumtegemea Allah.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

KILELE CHA TAMASHA LA MICHEZO JAMIA AHMADYYA 2024

Kutoka uk. 01

vile kuvuta kamba,
mirudaba, bari(center), mbio za kupokezana vijiti, mpira wa meza, mpira wa wavu na Mpira wa miguu. Na michezo ya mtu mmoj mmoja ni kama vile Riadha mita 100, mita 1600, mbio za miguu mitatu, kichurachura, kulenga shabaha, kuruka juu na chini, kurusha tufe, kurusha mkuki n.k.

Katika mashindano ya kitimu, timu ya Shaja'at iliibuka mabingwa kwa kushika nafasi ya kwanza na kufuatiwa na timu ya Shafqat iliyoshika nafasi ya pili. Na kwa mashindano ya mtu mmoja mmoja Mwanafunzi Mubarak Abdallah ameibuka kuwa mshindi wa kwanza kwa kushiriki mashindano mengi na kushinda.



HAFLA YA UGAWAJI WA ZAWADI

Siku ya tarehe 10 Oktoba 2024 ilikuwa ni kilele cha mashindano hayo ambayo yalihitimishwa kwa hafla maalumu ya kugawa zawadi kwa washindi mbalimbali. Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Amiri na Mbashiri mkuu hapa nchini Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad sahib.

Hafla ilianza majira ya saa 4:00 asubuhi kwa usomaji wa Kuran Tukufu iliyosomwa na Hafidh Abdurrahman Lundo na kufuatiwa na shairi la Kiarabu lililosomwa kwa pamoja na Ismail Pembe, Abuswidiq Pembe na Suleiman Abdallah. Baada ya shairi hilo ilifuata ripoti fupi ya michezo iliyosomwa na Mwl. Hussein Mpenda Sahib. Baada ya ripoti hiyo fupi, Mheshimiwa mgeni rasmi alikabidhi zawadi kwa washindi mbali mbali.

Katika hotuba yake ya kufunga tamasha la michezo, Amir sahib alimpongeza sana mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya na timu yake kwa kuandaa vyema mashindano hayo.
Pia aliwakumbusha wanafunzi ya kuwa lengo la mashindano hayo ni kuwafanya wawe imara na kama alivyosema Mtume Mtukufu[Saw] ya kuwa, "Mu'min mwenye nguvu ni bora kuliko aliye dhaifu."
Hivyo aliwataka wanafunzi watumie mashindano haya na yajayo kwa ajili ya kuimarisha afya zao. Akielezea falsafa ya shindano la mbio za kupokezana vijiti, Amir sahib alisema, shindano hili linaakisi hali halisi ya historia ya kiislam, alisema kijiti kilianza kwa Mtume mtukufu[saw] na baada yake kwa makhalifa wake, kisha kwa Hazrat Masih Mau'ud a.s na baadae kwa Makhalifa na kutufikia sisi. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa kijiti hiki hakianguki chini. Aidha Amir Sahib amekumbusha kauli ya Khalifa Mtukufu[atba] aliposema kuwa kila kitu kina haki yake, na haki ya mwili ni mazoezi, ukifanya mazoezi mwili utakuwa imara na ndipo utaweza kufanya kazi ya jumuiya kwa ufanisi.


Baada ya hotuba hiyo ya Amir sahib, Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti mkuu wa chuo cha jamia Ahmadiyya na Naib Amir hapa nchini, alimshukuru sana Amir sahib kwa kukubali mwaliko na kufika katika hafla hiyo na kupongeza jitihada zinazofanywa na wanafunzi katika nyanja mbalimbali.



SHEIKH MUHAMMAD MUNAWAR SAHIB

NA USHAURI WA MWANA ALIYEAHIDIWA[ra]

Na; Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Kiwalani Dar es Salaam



Tarehe 12 march 1916, Hazrat Mirza Bashir-u-Din Mahmood Ahmad (ra) mwana aliyeahidiwa Khalifatul Masih wa II alitoa muhadhara ukiwa ni ushauri kwa wabashiri. Muhadhara huo hatimae ulichapishwa katika sura ya kitabu na kupewa jina- Ushauri kwa wabashiri, ilikuwa ni desturi ya Khalifatul Masih kukutana na Mubashir au wabashiri kabla ya kwenda kwenye vituo walivyopangiwa.

Maneno yaliyoandikwa na yale unayoyasikia kutoka kwa Khalifa wa Allah kuna tofauti. Sheikh Muhammad Munawar alipata faida zote mbili alimsikia Khalifatul Masih wa II[ra] akimpa ushauri huu na aliweza kupatiwa Kitabu-ushauri kwa wabashiri. Wabashiri wawili walikuwa wamemaliza masomo yao, Sheikh Abdul Karim Sharma na Sheikh Muhammad Munawar tayari walikuwa wamekwisha fanya kazi katika sehemu kadha wa kadha za kidini katika India. Kwa mara ya kwanza walikuwa wanatoka katika bara la Asia na kukanyaga Afrika.

Ulikuwa ni mkutano wa baraka sana kuagana na Khalifatul Masih wa II. Sheikh Muhammad Munawar alikwisha jipatia baraka ya kufundishwa Kuruani Tukufu na tafsiri yake na aliyekuwa Profesa katika chuo kikuu cha wabashiri na mkuu wa chuo hicho Hazrat Mirza Nasir Ahmad, mwana wa Khalifa wa II[ra] Hafiz wa kuruani Tukufu na mhitimu wa M.A kutoka katika moja ya vyuo bora duniani Oxford, vingine viwili ni Cambridge na Havard.

Masheikh hawa wawili walifika kwa Khalifatul Masih wa II na kupata bahati hiyo ya kuagana na kiongozi wa kiroho, Sheikh Muhammad Munawar alikuwa na karatasi na kalamu na hakutaka hata neno moja limponyoke. Tutaendeleza ushauri huo alioutoa Khalifatul Masih wa II (ra) kwa masheikh hao na tutachunguza ni kwa kiasi gani katika maisha yake ya ubashiri, Sheikh Muhammad Munawar alijitahidi kuyatekeleza.

•Usafishaji wa nafsi ni jambo la awali. Jitihada zifanyike za kusafisha nafsi na njia hizi ni pamoja na:-

1) Usiache sala kwa sababu ya shughuli yoyote uliyonayo. Kwanza sali kwa wakati na hata kama uko kwenye mahubiri acha na uende kusali, waombe radhi na wasipoelewa usiwajali wewe timiza wajibu wako. Njia ya mafanikio ni hiyo, Huzur alitoa mfano unaoeleza umuhimu wa Sala na kuacha chochote kile unachokifanya sawa na masimulizi ya historia, masahaba sitini elfu wa Mtukufu mtume Muhammad[saw] wakiongozwa na Khalid bin Walid walishiriki katika vita ya Yermuk dhidi ya wakristo milioni moja. Inasemekana Mkwe wa HERELIS ndiye alikuwa kiongozi wa jeshi la adui. Wakati wa vita alimtuma jasusi ili kufanya utafiti na uchunguzi kuhusu waislam nini hasa wanachotegemea sana. Jasusi huyo alirudi huku amekata tamaa na kusema, Waislam hatuwawezi kuwashinda, alieleza kwamba wao wanaporudi kutoka vitani wanavua kofia na kuanza kukoroma. Waislam hata baada ya mchoko na kazi nzito walitumia usiku katika ibada za vilio wakimuomba Allah msaada. Hivi ndivyo masahaba walivyoonesha imani yao hata wakati mgumu hawakuacha sala. Waliokaa na Sheikh Muhammad Munawar wanaweza kutoa ushahidi ya kuwa hakuchelewa asilani kwenye sala hata mtu akichelewa kutoa adhana alitoka mwenyewe na kutoa adhana. Sala na wakati wake ni jambo ambalo alizingatia sana, Sheikh wa mkoa wa Kagera Sheikh Mikidadi alifika ofisini na ulikuwa mjadala, vitabu vimejazana zikitolewa nukuu kushoto na kulia kikizungumzwa kiswahili mara nyingine kiarabu, lakini adhana ilipotoka alimwambia Sheikh Mikidadi saa ya sala lakini Sheikh Mikidadi akasema tuendelee. Sheikh Muhammad Munawar alisema hatuwezi kuendelea wakati adhana imetoka.

Sheikh Mikidadi Yusufu alitishia kuondoka lakini Sheikh Munawar hakubadili msimamo. Sheikh Mikidadi Yusufu alitulia ofisini hadi mwisho wa sala na mazungumzo yakaendelea, Sheikh Muhammad Munawar alikuwa anakumbuka ushauri aliopewa na Khalifatul Masih wa II (ra) katikati ya shughuli yoyote acha shughuli hiyo ukafanye ibada. Hili ni somo kubwa tulilojifunza sisi tuliokuwa naye.

2)Jiepushe na majivuno. Katika mahubiri wanakuwa wapo watu unajenga hoja. Unambwaga unayajadiliana naye, kibinadamu taratibu kiburi kinaingia unajiona hodari unajiona mjuaji. Unapokuwa kwenye mjadala fanya sana istighfar, Allah Akuepushie na yote yanayoweza kukutoa kwenye nyumba imara ya taqwa. Jambo hili la Istighfar Aliwakumbusha masheikh na walimu kwani kinachofanikisha ni ukweli wa Islam kwa watu wote kwa upole, huruma na mapenzi.

3)Tahajudi: katika siku kuna uchafu mwingi unaokusanya, unahitaji kuusafisha mwili na cha kusafisha uchafu wote huo ni sala ya Tahajudi. Sisi tuliokuwa tunakaa msikitini tulikuwa tunasikia vilio usiku na kweli ukiamka unakuta taa inawaka na hapo sisi tunasema Sheikh yuko kazini.

4) Kufunga saumu: kufunga kunaondoa kutu kwenye moyo. Mwalimu Khamis Sultan Wamwera aliyefanya kazi na Sheikh Muhammad Munawar anaeleza ya kwamba Maulana alikuwa na desturi ya kufunga mara kwa mara.

5) Tenga muda wa dakika kumi na tano au ishirini kutafakari kumkumbuka Allah. Hii ni desturi ya wachamungu na imeleta mabadiliko makubwa. Kujitenga ukiwa peke yako ni jambo jema, mtukufu mtume Muhammad[saw] alikuwa anakwenda kwenye pango nje kidogo ya Maka na akikaa huku kutafakari. Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alikwenda Hoshiarpur na huko aliomba na kupata habari njema za kuzaliwa kwa mwana Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Bashir-u-din Mahmood Ahmad (ra). Nabii Isa (as) alijitenga na kuwa Jangwani siku Arubaini.

6) Muhimu kusoma sana tena kwa mapana na marefu na uwe na desturi ya kununua vitabu na kujijengea maktaba: Sheikh Muhammad Munawar alitekeleza agizo hilo la Khalifatul Masih wa II kwa kiwango kikubwa sana. Asubuhi kabla ya kuanza kazi anasoma Kuruani Tukufu na kunipatia fedha nikanunue magazeti. Hakuwa anachagua magazeti ya kusoma, yote yaliyokuwa yanachapishwa siku hizo Daily News, Sunday News, Uhuru, Mzalendo, Mfanyakazi, The Nationalist, Kiongozi, Ngurumo, Mwafrika yote hayo yalinunuliwa na kuyapitia kwa makini. Mahali popote palipohitaji majibu, maelekezo, ufafanuzi alifanya hivyo. Uwezo wake wa lugha ya kingereza na

Endelea Uk wa 5..

SHEIKH MUHAMMAD MUNAWAR SAHIB

NA USHAURI WA MWANA ALIYEAHIDIWA[ra]

Kutoka Uk>04

kiswahili ulikuwa mkubwa sana. Aliweza kutoa maelezo au jibu kwa gazeti la Daily News bila matayarisho yoyote. Yeye alipiga kwenye mashine yake moja kwa moja na humo usingekuta kosa la lugha. Ni jambo la kufurahisha ya kwamba hizo lugha alizozifahamu alipenda na watu wengine wazifahamu. Alikuwa na darasa la kiarabu kila baada ya magharib. Mimi hakunipangia muda wa kusoma. Akiwa ofisini naanza kusoma Yasarnal Qur'an wakati huo yeye anaendelea na kazi zake na kunisikiliza. Ni yeye ambaye alinijengea msingi mzuri wa kingereza. Katika miaka hiyo ya sabini watu hawakuwa wengi msikitini wakati mwingi palikuwa kimya, na wakati Sheikh Muhammad Munawar anatoka ofisini kwake, kulikuwa na mkungu anakaa nje na kuanza kujisomea. Sheikh alipenda sana kusoma na hakufurahia hata kidogo kukuona huna kitabu. Alinipatia vitabu vingi vya kingereza vya jamaat na akanihimiza nivisome na nikamuuliza maneno yoyote magumu ambayo sikuwa nayaelewa na hakuchoka katika kuelezea. Kusoma ndio kilikuwa kikombe chake cha Asali.

Alisoma vitabu vya kila aina hata riwaya za kingereza alizisoma kwani sawa na maelekezo ya Khalifatul Masih wa II (ra) hii ndio njia ya kufahamu utamaduni wa watu. Alikuwa anatoa mfano wa khalifatul Masih wa I Hazrat Maulvi Alhaj Noor-din (ra) ambaye alikuwa amesoma kazi zote za William Shakespeare. Kuhusu kusoma alipenda kuuliza unasoma kitabu gani Na aliomba umueleze kwa muhtasari yaliyomo.

Baadae nilikuja kugundua kuwa Khalifatul Masih wa IV Hazrat Mirza Tahir Ahmad[ra] alikuwa mpenzi mkubwa wa fasihi na alikuwa amesoma riwaya nyingi za kingereza . Kwenye kitabu chake cha Gulf Crisis anamnukuu William ShakesPear katika tamthilia yake Macbeth na kuna mahali anapomnukuu Mshairi maarufu wa Marekani Robert Frost na Ghalib.

Kuhusu kusoma alipenda kuuliza unasoma kitabu gani na alipenda umueleze kidogo maudhui ya kitabu, tangazo lilitolewa msikitini kwamba yeyote atakayekutana na gazeti au Kitabu vinaeleza juu ya Ahmadiyya basi kama ana pesa anunue na atarudishiwa na kama hana basi aje ofisini achukue pesa na kitabu hicho au gazeti hili linunuliwe. Kwa njia hii vilinunuliwa vitabu vingi na vilivyokuwa na makosa waliandikiwa wachapaji ili waelewe makosa yaliyo katika hicho walichochapisha.

Hali hii ya Sheikh Muhammad Munawar kupenda kusoma iliwaambukiza wengi wakawa na furaha ya kueleza kitabu walichosoma na yale waliyoyakuta katika kitabu hicho. Hali hii ilijenga sana utamaduni wa kupenda kusoma Ndio maana mazungumzo ya siku hizo yalizunguka kwenye kitabu ulichosoma.

7) Mubashiri ni Mtumishi ana heshima kwa sababu anawakilisha chanzo cha heshima zote. Sheikh Muhammad Munawar kwa kweli na uhakika alijtolea sana katika kuwatumikia wananchi, wasiwasi ulikuwa unampata kama hakuoni siku mbili tatu ataulizia mpaka apate habari zako. Hakupenda kukaa ofisini tu, hapana alipenda kutoka nje kuwafuata wananchi wake. Alikuwa ni mtumishi aliyeheshimika sana , kuna siku alitoka kwa basi kwenda Rufiji, kufika mwisho wa safari watu walianza kushuka lakini kwa sauti moja abiria walisema ngoja kwanza Sheikh huyo ashuke. Na alipoteremka chini na kilemba chake alitoa Assalam Alaykum iliyoitikiwa na wote. Aliwahi pia kufunga safari ya Mahuta, wanajamati walikuwa na wasiwasi atalala wapi na atakula nini aliwatoa wasiwasi kabisa kuhusu malazi na chakula, nitakula kile kile mnachokula. Baadhi ya wahindi wa Mahuta walitaka aende kulala kwao alisema yeye atalala kwa ndugu zake wa kiroho na kila mikutano ya Jalsa iliyokuwa inazunguka katika mikoa alikuwa anahudhuria na alisema asipewe mahali maalum pa kulala, yeye angeliweza kulala mahala popote walipolala wanajamati.

Hakukosa kuwatembelea wagonjwa na waliopata matatizo, vijana ambao hawakuwa na karo waliweza kusaidiwa. Alipenda sana nchi na alisema hakuna katika sala zake aliposahau kuiombea nchi aliyoanza kuitumikia toka uhuru haujapatikana. Mimi sikuwahi kwa miaka yote niliyoishi naye kumuona na nguo yoyote ile isipokuwa nguo hizo nyeupe za kipanjabi ambazo alizivaa kila siku.

Hata wakati vitu vimeadimika mafuta ya kula, sabuni hata dawa ya meno, sheikh Muhammad Munawar hata siku moja hakulalamikanaingawajechakula chake kikuu kilikuwa chapati. Aliweza kula kilichopatikana kwa furaha na kuridhika.

Katika utumishi wake hakuwa na woga alisema kweli na kutetea mafundisho ya Islam ilipotakiwa kufanya hivyo. Muswada wa sheria wa ndoa uliotaka mtu ukishakaa na Mwanamke miaka miwili amekwisha kuwa Mke alipinga na kuandika uliotawanywa kwa wabunge, hilo alisema ni kuendeleza ufuska nchini. Kuhusu pombe ingawaje inaonesha kuleta faida lakini ilikuwa na madhara makubwa kwa taifa. Si sawa kuweka Umri kadhaa wa binti kuolewa kipimo ni kuvunja ungo. Nyumba za dini zilipochukuliwa alipeleka malalamiko yake moja kwa moja hadi Ikulu na kweli nyumba za dini zilizokuwa zimetaifishwa zikarudishwa katika shughuli zake hizi za kuwatumikia wananchi.

Alikuwa anamtanguliza Allah na hakusahau maombi aliyoambiwa na Khalifa wa II Hazrat Mirza Bashir-u-din Mahmood Ahmad[ra] aombe kila mara-E Mola wangu nakuomba nisiwatoe watu kwenye njia iliyonyooka. Kuanguka kwa Kiongozi ni jambo kubwa.

Akakumbuka kisa kimoja alichopewa. Siku moja mvua ilikuwa inanyesha na Imam akamwambia Mtoto nenda taratibu usianguke, Yule mtoto akasema usijali kuanguka kwangu, jali sana kuanguka kwako kwani kuanguka kwako jamii nzima itaanguka.

8) Usiseme bila kutafakari: Kwa ufasaha wake wa lugha Sheikh Muhammad Munawar alikuwa bingwa wa kuchagua maneno. Jitihada kubwa aliifanya ya kufahamu lugha na utamaduni wa watu. Hii ilimsaidia hata kupenyeza utani pahali panapofaa. Siku moja bwana mmoja alitoka Muhimbili kung'oa jino akaja kumsalimu ofisini na akamueleza juu ya kung'oa jino, Sheikh Muhammad Munawar alimwambia nini bwana haifai kung'oa meno, hayo hukupewa ule muhogo bali kusoma Kuruani Tukufu. Hotuba zake zilikuwa na mvuto wa ajabu kwa sababu ya umahiri wake wa kuchagua maneno yanayofaa wakati unaofaa. Singoro Marijani alipoandika kutupinga sisi, alimpa jibu tamu lenye anwani-Takataka za songoro marijani ni mbolea kwetu.

Hayondiyomaagizoyaliyomfanya Sheikh Muhammad Munawar afaulu sana katika kutekeleza majukumu yake.

Bustani ya Washairi

NGAO

Bila mapenzi na hofu, manya muhali kupona
Hizi siratwa tukufu, kumfikia Rabana
Zikiepusha uchafu, na bahari ya fitina
Mapenzi pamwe na hofu, ni ngao ya kukulinda.

Mahmood Hamsini Mubiru (wa Mamba)
==========

DUA

Ewe Mola Mtukuka, Rabi nakusujudia.
Ndiye Wewe Msifika, utakalo hutukia.
Ulinzi wako nataka, kwa dua kumtakia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Peke hawezi ongoka, pasi kumsaidia.
Ni Rehema wa hakika, binti ulonipatia.
Leo sabaa miaka, amekwisha ifikia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Mzuri mwenye fasaha, fundi wa kusimulia.
Wala si mwenye karaha, tabiaze zavutia.
Manani mjaze siha, na umbo la kuvutia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Rabi mwepushie dhiki, kwa nuru muangazia.
Na pale penye visiki, Rabi tamsafishia.
Na njia usiidhiki, apite kwa kutulia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Nakuomba Mola wangu, huku nakuhimidia.
Bariki binti yangu, abaki Ahmadia.
pia khalifa wa Mungu, asije mpuuzia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Elimu ya kufururika, muwezeshe kubukua.
Hata huko Amerika, aende kuichukua.
Na dini yako hakika, asije kuisusia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Hata niwe taabani, dua nitakufanyia.
Uwe mcha Rahamani, Mola Taala Jalia.
Nitakuwa furahani, dini ukitumikia.
Mola wangu muongoa, peke hawezi ongoka.

Rajabu Mkieti Abasi
Al wattan mlezi
14-10-2024

Kitendawili

Anapenda kuoga, uji kwake adui
Wadudu yeye mwoga, michezo hatulii
Anazikula mboga, kimwimbia halii
Wamjua ninani, mwenye kitendawili?

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

KANZU

Kanzu imechanwa nyuma, na siri imefichuka
Ndio kaida adhima, kabainisha Rabuka
Na hila za kina Mama, ufanye kuziepuka
Kaida huna adhima, keti na kutafakari

Mahmood Hamsini Mubiru(wa Mamba)
==========

Kasida ya kumsifu Mtume Mohamed (saw)

19

فدم الرجال لصدقهم في حبهم
تحت السيوف أُريق كالقربان

Tafsiri: Hivyo damu ya watu ikamwagiwa chini ya panga kama dhabihu kwa sababu ya uhalisi wa upendo wao

Maelezo: Masahaba wa Mtume Mtukufu (saw) walionesha ikhlasi na moyo wa upendo kiasi kwamba hawakusita kujitolea mhanga njiani kwa Allah. Sababu pekee iliyowapelekea kufanya hivi ni mahaba na upendo kwa Mola wao na Mtume wake (saw). Kutokana na upendo huo hawakujali hata maisha yao bali walitoka kifuambele ili kuitetea dini tukufu ya Uislamu.

20

جاؤوك منهوبين كالعريان
فسترتهم بملاحف الإيمان

Tafsiri: Walikujia wakiwa wamenyang'anywa (mali yote) kana kwamba walikuwa rabana nawe ukawafunika kwa mashuka ya imani

Maelezo: Masahaba walipojiunga na dini tukufu ya Uislamu waliachwa na ndugu na jamaa zao. Kwa kweli hali hii ilikuwa ngumu kwao kana kwamba walinyang'anywa mali zao zote. Lakini waliendelea kupata maarifa ya kidini kwa Mtume Mtukufu (saw) walipata nuru ya imani iliyowafunika na kuwatunza. Nuru hii ilisababisha wamkurubie Allah subhanahu wataalaa na wakapewa jina la *Ashabii kan-nujuum*.

21

صادفتهم قوماً كروثٍ ذِلةً
فجعلتهم كسبيكة العقيان

Tafsiri: Uliwakuta watu (wenye hali) duni kama mavi na ukawageuza kuwa kipande cha dhahabu safi

Maelezo: Masahaba wa Mtume[saw] walionesha mabadiliko makubwa sana katika maisha yao. Kabla ya kujiunga na dini tukufu ya Uislamu walikuwa wakifuata mazoea ya kijinga lakini baada ya kupata malezi bora kwa Mtume Mtukufu (saw) thamani yao ikaongezeka. Walikuwa wenye faida kubwa kwa watu wengine na hata sasa watu wanaendelea kuiga mifano yao ili kuleta mageuzi katika maisha yao.

22

حتى انثنى بزّ كمثل حديقة
عذب الموارد مثمر الأغصان

Tafsiri: Hata pori zikageuka kuwa kama viunga vyenye chemchemi tamu na matawi (ya miti) yenye matunda

Maelezo: Katika ubeti huu hali ya maisha ya masahaba kabla ya kujiunga na Uislamu imeelezwa kama pori kusiko na ustaarabu. Baada ya kuongoka maisha yao yaligeuka kama bustani ambako chemchemi za maji matamu ya kiroho zinabubujika na kurutubisha miti inayozaa matunda mengi. Miti na matunda ya Kiislamu ni watu ambao bado wanaendelea kupata nguvu kutoka mafundisho ya Uislamu na kuyasambaza duniani.

23

عادت بلاد العرب نحو نضارة
بعد الوجى والمحل والخسران

Tafsiri: Mataifa ya kiarabu yakaelekea kustawi baada ya hali ya ukavu, ukame na uharibifu.

Maelezo: Hali ya Bara Arabu kabla ya ujio wa Uislamu ilikuwa mbaya sana. Watu walienda mbali sana na dini na walizidi katika madhambi na maovu. Uharibifu wa kila aina ulienea na ukapelekea maji ya kiroho kukauka au kukosekana. Katika hali kama hii ikaja dini tukufu ya Uislamu na watu wakaona mabadiliko katika hali zao za kidini. Kwa kweli ustawi ukapatikana.

24

كان الحجاز مغازل الغزلان
فجعلتهم فانين في الرحمان

Tafsiri: Watu wa Hijazi walikuwa ashiki wa wanawake warembo, nawe ukawafanya wakijipoteza katika Rahmani

Maelezo: Kabla ya ujio wa Uislamu, watu wengi walizama katika mambo mabaya. Mtume Mtukufu (saw) aliwaelekeza na kuwafundisha kwamba Mungu ni mmoja apaswaye kuabudiwa; ambaye ni mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu; ambaye ni mtoaji wa riziki; aondoaye shari zote na aletaye heri zote. Hivi twapaswa kumwabudu Yeye pekee na kutekeleza maamrisho yake.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Hadithi ya Hamasa ya Kiislamu:

Jifunze kutokana na Makosa

Siku moja yenye baridi kali katikati ya majira ya baridi kali kundi la chungu lilikuwa na shughuli nyingi za kukausha nafaka fulani, ambazo zilikuwa na unyevunyevu wakati wa hali ya hewa ya vuli yenye mvua.



Panzi akiwa amepatwa baridi na njaa, alimjia mchwa mmoja. “Tafadhali nipatie punje moja au mbili kutoka kwa duka lako la mahindi ili kuokoa maisha yangu,” alisema kwa unyonge. "Tulifanya kazi usiku na mchana ili kuingiza mahindi haya. Kwa nini nikupe?" aliuliza kwa hasira kidogo. "Ulikuwa unafanya nini msimu wa joto uliopita wakati unapaswa




kukusanya chakula chako?"

Ah, sikuwa na wakati wa mambo kama hayo, panzi alisema. "Nilikuwa na shughuli nyingi sana nikiimba na nisingeweza kubeba mahindi."

Chungu alicheka bila huruma. "Katika hali hiyo unaweza kuimba majira yote ya baridi," alisema. Na bila neno lingine alirudi kwenye kazi yake.

Uislamu unatufundisha kwamba tunapaswa kuwasaidia wasiojiweza. Lakini pia inatufundisha kwamba tunapaswa kufanya kazi kwa bidii na si kutegemea fadhili za wengine kwa mahitaji yetu ya kila siku.

Unganisha Nukta kupata Mchoro



MAPISHI YA NDIZI MZUZU (MBIVU) ZA NAZI

Mara nyingi tunakula ndizi mzuzu za kuchemsha, ukijaribu mapishi haya unaweza usile tena mapishi ya kawaida ya ndizi mzuzu. Utamu wake ni wa kipekee na hiki ni chakula bora, na hakina vikorombwezo vingi.

Mahitaji

Nazi 1
Ndizi mzuzu zilivoiva 6
Sukari kijiko 1 cha chai
Hiliki



Maelekezo

Menya ndizi na zikate kwa urefu ili utoe ule uzi mweusi katika kiini cha ndizi. Usitupe maganda. Menya hiliki na kisha zitwange.

Kuna nazi na uchuje tui zito na jepesi. Katika sufuria ya kupikia, panga maganda ya ndizi mzuzu,vizuri na kisha juu yake panga ndizi kwa ufasaha.

Bandika sufuria jikoni na kisha weka tui jepesi. Acha kwenye moto ichemke hadi tui likauke.

Nyunyizia sukari kidogo kwenye ndizi na weka hiliki. Weka tui zito kisha acha lichemke kwa moto mdogo sana hadi tui likauke.
Unaweza kuepua na kujiramba.

ALLAH Ametuamrisha yafuatayo:

1. Fa tabayyanu
Ukipata taarifa, chunguza kwanza, tusijekuamini mambo yasiyo na ukweli yanayosambazwa juu ya wenzetu.

2. Fa aslihu jaribu kila
iwezekanavyo, kupatanisha ndugu, wakiwemo Waislam, na binadamu wenzetu.

3. La yaskhar
Tusifanye maskhara; utani unaoumiza nafs za wenzetu; inawezekana wao wakawa bora kuliko sisi mbele ya Allah SWT.

4. Wa la Talmizu
Tusitukanane. Tusivunjiane heshima. Tusidharauliane.

5. Wa la Tanabazu
Tusiitane kwa majina ya kejeli; yenye dharau; yanayodhalilisha.

6. Itnajibu kathiiran min aldan
Tujitahidi kuepuka shaka juu ya wenzetu. Tuepuke kuamua wenzetu ni wakosaji, wakati hatuna uhakika wowote.

7. Wa Aqsitu
Tuwe na mizani ya haki tunapoamua ugomvi au mzozo baina ya watu.

8. Wa la tajassasu
Tusichunguzane. Tusifanyiane ujasusi. Tusitiriane.

9. Wa la Yaghtab
Tusisengenyane. Tusizushiane maovu.

Sura Al Hujurat

Inna Allah yuhibbul mutatahirina

Mwenyenzi Mungu hupenda wanaojiweka wasafi kuepuka dhambi.
Ameen

Maelekezo ya maisha katika Qur›an

1_Usizungumze kwa ukali (3:159)

2_Jizuie na hasira (3:134)

3_Kuwa mwema kwa wengine (4:36)

4_Usiwe mwenye kiburi(7:13)

5_Samehe wanaokukosea (7:199)

6_Zungumza na watu kwa upole (20:44)

7 _Shusha sauti yako (31:19)

8_ Usiwakejeli wengine (49:11)

9_Watendee wema wazazi wako (17:23)

10 _Usiseme maneno ya kuwakosea adabu wazazi wako (17:23)

11_ Usiingie chumba cha wazazi wako bila kuomba idhini (24:58)

12_Andikishianeni mnapokopeshana (2:282)

13Usifuate rai ya yeyote kibubusa (2:170)

14_Muongezee unayemdai muda wa kulipa deni kama ana hali ngumu (2:280)

15_ Usile riba (2:275)

16_ Usijihusishe na rushwa (2:188)

17_ Usivunje ahadi (2:177)

18_Tunza amana (2:283)

19_ Usiufiche ukweli unaoujua (2:42)

20_ Wahukumu watu kwa haki (4:58)

21_Simamia haki (4:135)

22_Mali za marehemu zigawiwe kwa warithi wao (4:7)

23_Wanawake pia wana haki yakurithi (4:7)

24_Usile Mali ya yatima (4:10)

25_ Watunze yatima (2:220)

26_Msiliane Mali zenu kwa dhuluma (4:29)

27_Patanisheni miongoni mwa wanaogombana (49:9)

28_Jiepushe nakuwajengea watu Dhana mbaya (49:12)

29_ Msipelelezane na msisengenyane (2:283)

30_Msipelelezane au msisengenyane (49:12)

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

MATUKIO KATIKA PICHA







Sherehe ya ufunguzi wa kozi ya michezo ya mwaka kwa wanafunzi wa Chuo kikuu cha #Ahmadiyah nchini #Tanzania





Amir Sahib jamaat Tanzania akihutubia katika hafla ya Sirat un Nabii, huko Tegeta Dar es Salaam. Siku ya Jumapili 27 - Oktoba - 2024.



Maswali kutoka katika kitabu cha

MHISANI KWA UBINADAMU

Imetayarishwa na.
Sheikh Ali Dino Tahir - Simiyu

Ni muhimu , msomaji asome kitabu cha Mhisani… mara mbili na kuyatafuta majibu kutoka katika kitabu (Atfal,Khudam na Nasirat wa Simiyu huwa wanahifadhi Maswali na majibu hayo na kufanya mashindano kila wiki).

Uk. iii 1. Taja jina la mwandishi wa kitabu cha MHISANI KWA UBINADAMU?
Jb. Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad Khalifatul Masih wa pili Radhiallahu Anhu

2. Kitabu cha Mhisani kwa Ubinadamu ni mkusanyiko wa vitabu gani?
Jb. Vitabu vitatu 1. Mhisani wa Dunia 2. Rehema kwa ulimwengu wote 3. Mfano kamili

Uk.1, 2 3. Khalifa mtukufu alisema kwamba tuwaheshimu viongozi, na tusiwakashfu, viongozi wa aina gani
Jb. Khalifa Mtukufu alisema tuwaheshimu viongozi wa dini zote ambao kaumu zao zinakiri kwamba wao waliteuliwa na Mwenyezi Mungu.

4. Kwanini tuwaheshimu viongozi wa dini zingine?
Jb. Kwa sababu ni agizo la Allah mtukufu na si chaguo letu binafsi.

Uk. 4 5. Ni nani haswa anatakiwa ashiriki katika mikutano ya maulidi yaani mikutano ya Siratunnabi SAW?
Jb. Wanatakiwa washiriki waislamu na wasiokuwa waislamu katika mikutano ya maulidi

6. Kwanini katika mikutano ya siratunnabi wawe washiriki wasiowaislamu?
Jb. Ili wajue sifa njema za mwanzilishi wa Islamu na ufa na ufarakano kati yao na ya waislamu utoweke.

Uk 5 7.kuna faida gani watapata Waislamu wakihudhuria mikutano ya sira ya Mtume SAW?
Jb. Wakisikia sifa njema za Mtume Muhammad SAW mara kwa mara wataziiga tabia zake na imani yao itaimarika

8. Wasio waislamu wanaomtusi Mtume Muhammad SAW Sababu kubwa ni ipi?
Jb. Kwa sababu wasio waislamu hawajawahi kusikia kuhusu khulka zake njema ,tabia yake na hali yake ya maisha ilivyo sahihi.

Uk.7 9. Hadhrat Sayyidina Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad Khalifatul Masih wa pili R.A, alichagua madhmuni matatu kwa ajili ya hotuba ya Siratunnabi SAW aliyotoa 17 Juni 1928... Madhumuni matatu yale ni yapi.
Jb. 1. Hisani ya Mtume SAW 2. Kujitolea kwa Mtume SAW 3. Utakatifu wa Mtume SAW

10.Kamilisha sentensi "Mtume SAW aliambiwa na Mungu kwamba Dunia imefanyiwa hisani....."
Jb. Kupitia wewe (yaani Mtume SAW)

Uk 16 11. Badhi ya wakati kujitolea kunakuwa kubaya, toa mfano.
Jb. Mtu fulani alikuja na kujiunga na jeshi la Kiislamu akawa anapigana kwa ushujaa kabisa. Baada ya kumuona hivyo watu walisema kuwa huyo amepigana vita kwa ujasiri kabisa. Lakini Mtume saw akasema huyo ni mtu wa motoni. Baada ya kuisikia kauli hii, watu hao walishangaa sana .Na mtu fulani akamfuatilia (huyo mpiganaji) alimuona akiumia na jeraha na alimuuliza ni sababu gani iliyokufanya upigane vita? Basi akajibu kwamba "Mimi napigana kwa sababu nina bughudha na watu hawa." Kwa kuwa nia yake haikuwa kupigana kwa ajili ya ukweli na kupata radhi ya Allah kwa hiyo kitendo chake kimekuwa kisichokubaliwa.

Uk.19 12. Mambo gani Mtume Muhammad SAW alikuwa hayapendi kwa ajili yake.
Jb. Mtume Muhammad SAW hakupenda Mamlaka wala umashuhuri hata siku moja

13. Mtume Muhammad SAW alipopata wahyi wake wa kwanza alienda kwa nani?
Jb. Mtume SAW alipopata wahyi wake wa kwanza alienda kwa Waraka bin Naufal

14. Warka bin Nofel alikuwa ni dini gani Jibu. Alikuwa mkristo

15. Kwanini Bi Khadija RA alikuja na Mtume Muhammad SAW kwa Waraka bin Naufal?
Uk.20 Jb. Hadhrat Khadija alikuja na Mtume SAW kwa Waraka ili wapate ushauri kwake

16. Warka bin Nofel alipomsikiliza alimwambia nini?
Jb. Watu wako watakufukuza nchini, Laiti wakati huo ningekuwa kijana na kukusaidia

17. Mtume Muhammad[saw] alipomsikiliza Warka bin Nofel kwamba watu watamfukuza, Mtume alisemaje katika lugha ya kiarabu.
Jb. Mtume[saw] Alisema Awa Mukhrijiyya hum (Daima nimekuwa nikiwatakia mema watu hawa na kuwatendea mazuri, sasa hao watawezaje kunifukuza).

Uk.21 18. Mtume Muhammad SAW alitoa madai ya unabii baada ya miaka mingapi ya ndoa yake? Jibu. Baada ya miaka 15

Uk 22,23 19.Bi Khadija RA alikuwa ana rai gani juu ya mumewe alipodai utume?
Jibu. Bi Khadija alisema
كلا والله ما يخزيك الله ابداء إنك لتصل الرحم، وتحمل الكل، وتكسب المعدوم، وتقري الضيف و تعين على نوائب الحق
Hapana Hapana, kwa haki, Mwenyezi Mungu Hatakuacha uangamie Abadan. Wewe ni mwenye kuwatendea wema ndugu na jamaa zako. Hakuna yeyote aliyekujia akiwa ameelemewa ambaye hukumtua mzigo wake. Umezihuisha uarabuni sifa zile njema zilizokuwa hazipo. Hakuna msafiri yeyote aliyekujia ambaye hukumkirimu na hakuna yeyote aliyepata msiba unaojuzu ambapo wewe ukawa hauko tayari kumsaidia.

Uk 24, 25 20. Rafiki yake Mtume SAW aliyekubali madai yake mara moja bila ya kusita,anaitwa nani?
Jb. Hadhrat Abubakar Sadiik Radhiallah Anhu

Uk 25 21. Taja majina ya watu wa familia waliomuamini Mtume Muhammad SAW mara moja
Jb. Hadhrat Bi Khadija RA, Hadhrat Ali RA, Hadhrat Zaid bin Haritha RA (aliyekuwa mtumishi wake Mtume)

22.Taja jina la rafiki yake Mtume SAW aliyechelewa kusilimu miaka ishirini na moja? Jibu. Hakim bin Hizam

23. Hakiim bin Hizaam aliyekuwa baado hajasilimu alimnunulia nini Mtume SAW na kumpelekea hadi Madina
Jibu. Lilikuwa koti la thamani kubwa

Uk.26 24. Eleza tabia za Mtume Muhammad[saw] alipokuwa mtoto
Jb. Kijakazi wa Abu Twalib anasema, wakati akiwa mdogo alipokuja nyumbani kwa baba yake mdogo Abu Twaalib, basi watoto wote walikuwa wakigombana gombana, lakini yeye hakushiriki asilan katika mambo hayo. Watoto wote walipokuwa wakiona vyakula walikuwa wakivikimbilia, lakini yeye alikuwa hata havitazami. Alikula chochote alichokuwa akipewa, mwenyewe alikuwa haombi. Huu ni ushuhuda wa kujistahi kwake, kujiheshimu kwake na kutosheka kwake.

Uk.27,28 25. Katika kikao makafiri wa Makka waliposema kwamba tusambaze habari ya kwamba yeye (Muhammad) ni Muongo na mchawi, Nadhar bin Haarith aliyekuwa mpinga sana hoja zao, alisemaje kuhusu hilo?
Jb: Nadhar bin Harith alisimama na kusema kwa jazba kwamba: Lifikirieni jibu lenye kukubalika akilini. Muhammad SAW amezaliwa kati yenu, amekua kijana kati yenu, ninyi nyote mlikuwa mkimpenda na mlikuwa mkizisifu sana khulka zake. Mlikuwa mkimfahamu kuwa yeye ni mkweli kuliko wote kiasi ya kwamba amezeeka na mvi zimemjia kichwani na ametoa madai anayoyatoa, sasa kama mtasema kwamba ni muongo, nani ataamini kuwa yeye ni muongo. Watu watakusemeni ninyi wenyewe kuwa ndio waongo.Liacheni jibu hili na mfikirie linguine.

Uk.28,29 26.Hadhrat Anas RA alikuwa mtumishi wa Mtume SAW tangia utotoni,yeye anasemaje kuhusu tabia ya mtume
Jb. Hadhrat Anas RA. Anasimulia kwamba hata kama niliharibu kazi kwa kiasi chochote kile, Mtume SAW hakuwa akinikasirikia asilan na wala hakuwa akinitazama kwa hasira. Kisha hakuwahi hata mara moja kuiagiza kuifanya kazi ambayo nilikuwa sina uwezo nayo na kazi yoyote aliyoniagiza kuifanya alikuwa akishirikiana na mimi kuifanya

29.. Qais bin Saib alikuwa nani
Jb. Qais bin Saib alishirikiana na Mtume katika Biashara

Uk,29,30 30. Qais bin Saib alisemaje kuhusu Mtume Muhammad SAW?
Jb. Qais bin Saib alisema kwamba Sijawahi kumuona mshirika mwema kama huyu hakuwahi kufanya udanganyifu wowote, hakuwahi kufanya utukutu wowote wala kugombana hata kidogo.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

HAIBA YA MFALME SULEIMAN AS

Kutoka uk. 12

na Imani kuwa Suleiman huenda alikuwa mtu wa ajabu aliyekuwa na vipawa vilivyopindukia uwezo wa kawaida wa kibinadamu.

Makala hii inakusudia kuangazia ukweli juu ya dhana na mitazamo mbalimbali inayozunguka haiba ya Suleiman na maisha yake.

UFALME WAKE

Suleiman alirithi Ufalme kutoka kwa baba yake, Daud (as) anayetambulika kuwa ndiye Muasisi wa dola ya Kiyahudi, shujaa mkuu wa Israeli na Mfalme mwenye nguvu na haiba kubwa. Daud (as) ndiye aliyeziunganisha koo zote za Kiisraeli kutoka Dani hadi Beersheba na kuasisi dola kubwa ambayo milki yake ilienea kutoka mto Furat (Euphrates) hadi mto Nile. Ushujaa wa Daud (as) ulidhihirika Zaidi alipowaongoza Waisraeli katika harakati za kutanua milki yao. Aliongoza na kushinda mapambano mengi makubwa ambayo baadhi yake yalionekana kuwa ni hatari hata kwa maisha yake mwenyewe. Hadi leo hii katika medani za siasa, Daud (as) anatajwa kuwa ndiye baba wa taifa la Israeli.

Baada ya kifo cha Daud (as), Suleiman alitawazwa kuwa Mfalme wa Israeli. Yeye alianzia pale alipoishia baba yake na kuendelea kuitanua Zaidi dola hiyo ya Kizayuni. Historia inaonyesha kuwa dola hii ilifikia katika kilele cha ustawi wake katika enzi za Suleiman wakati huo milki ya dola ya kizayuni ilitanuka hadi Kaskazini mwa Syria kwa upande wa Mashariki mwa bahari ya mediterrania na kuteremka hadi katika eneo la bahari nyekundu (Sham), Ufalme huo ulienea katika bara arabu hadi katika ghuba ya Uajemi.

Ni wakati wa Suleiman (as) ndipo dola ya Israeli ilipopiga hatua kubwa katika Nyanja za elimu, uchumi, utamaduni na hata ulinzi. Miongoni mwa alama kubwa za maendeleo ya kitamaduni zilizoachwa na Suleiman ni Hekalu lake lililopo Jerusalem (Masjid Aqsa) ambalo baadaye lilifanywa kuwa kibla ya wana wa Israeli. Hekalu hilo linaheshimiwa hadi sasa na limo katika orodha ya UNESCO kama mojawapo ya urithi wa dunia.

LUGHA YA NDEGE

Moja ya mambo yanayotamkwa kama maajabu ya vipawa vya Suleiman ni madai ya kwamba alijua lugha za ndege na wanyama. Hili ni jambo lililohubiriwa kwa shangwe kubwa na viongozi wa dini katika vizimba mbalimbali vya mahubiri yao. Baadhi yao hudiriki kurejea hata simulizi iliyomo katika Hekaya za Abunuwasi (kisa cha mtu aliyesikia lugha ya wanyama) kuwa kama ushahidi wa madai yao wakiamini kuwa mtu huyo si mwingine ila ni Nabii Suleiman bin Daud (as).

Dhana hii bila shaka inatokana na uelewa waliokuwa nao juu ya aya ya Qur'an Tukufu inayosema kuwa Daud na Suleiman walifundishwa lugha ya ndege (27:17). Lakini ukweli ni huu ya kwamba katika aya hii neno 'MANTIQAT TAIR' (lugha ya ndege) hayamaanishi lugha kwa maana ya mazungumzo yanayofanywa kwa kinywa na ulimi tu. Hapa neno 'MATIQ' lina maana pana Zaidi. Asili ya neno hili ni NUTQ ambayo maana yake hasa humaanisha mawasiliano ya kimaongezi kwa namna yoyote iwayo na si lazima kuwepo na matamshi. Kwa mujibu wa kamusi ya Mufradatur Raghibul Asfahaani neno MANTIQ humaanisha lugha yoyote inayoweza kutoa maana ya neno, iwe ya sauti, ishara, alama au maandishi.

Ifahamike ya kwamba kila kiumbe kina njia yake ya mawasiliano na mazungumzo. Neno 'kusema' katika lugha ya Kiarabu humaanisha ishara yoyote inayotumika na kiumbe husika kutoa taarifa juu ya jambo fulani. Badala ya kauli ya kinywa hali ya kitu pia huhesabiwa kuwa ndiyo kauli. Kuna usemi wa Kiarabu usemao; 'IMTALA'A ALHAUDHU WA QABLA QATNII' (Pipa lilijaa likasema imetosha) hapa haimaanishi kuwa pipa lilitamka, bali maji yakimwagika huwa habari imeshatambulika kuwa pipa limejaa.

Kama kuna uandishi uliotumia kwa uangalifu maneno ya lugha na maana zake basi bila shaka ni uandishi wa Qur'an Tukufu. Kwani Allah Anapozungumzia lugha za maneno ya kinywa na ulimi hatumii neno MANTIQ bali neno lililotumika juu ya lugha ya aina hiyo ni LISAN kama inavyoonekana katika sura 14:10 na 30:23. Lakini neno MANTIQ linahusishwa na lugha ambayo kila kiumbe bila kujali lina sauti au la linaweza kuzungumza. Ndani ya Qur'an Tukufu kunatajwa habari ya baadhi ya viungo vya watu kutoa ushahidi juu ya matendo ya mja. Na inafanyika hivyo kama uthibitisho ya kuwa Allah hukisemesha kila kitu na katika aya inayozungumzia jambo hili neno lililotumika ni ANTAQA ambalo lina asili moja na MANTIQ (41:22). Kwa hivyo haimaanishi kuwa ngozi zitaota vinywa zitamke la! Bali zipo njia za kuifanya ngozi iweze kutoa taarifa zinazohusu mwili husika.

MANTIQ AL TAIR KATIKA DUNIA YA LEO.

Nabii Daud na Suleiman kudai kuwa wamefundishwa lugha ya ndege, ilikuwa ni taarifa juu ya fani muhimu ya kielimu ambayo huenda haikuwapo duniani kabla yao. Ifahamike kuwa ndege na wanyama wanazo njia fulani za mawasiliano ambazo si rahisi kwa mwanadamu kuzitambua bila elimu maalum. Hali kadhalika zipo njia na kanuni ambazo kwazo mwanadamu anaweza kuwasiliana na wanyama na ndege. Katika jamii za wafugaji aghalabu elimu ya aina hii japo kwa kiwango kidogo hutumika katika uongozaji wa mifugo. Wanyama pia huweza kutoa ishara mbalimbali juu ya hatari iliyo karibu na hivyo kumfanya mchungaji wao kuchukua tahadhari.

Hii inaonyesha kuwa, wakati wa Suleiman yumkini ndio wakati ambapo wanyama na ndege walianza kutumika katika shughuli mbalimbali za kiserikali ikiwemo za ulinzi, upelelezi na hata usambazaji wa taarifa mbalimbali.

Huu ni utamaduni maarufu mno kwa sasa duniani. Katika nchi mbalimbali wanyama wamekuwa msaada mkubwa katika upelelezi na utafiti. Leo hii si jambo la kushangaza kuona mbwa, nguruwe, vyura, panya n.k walitumika katika majeshi ya ulinzi na usalama kwa ajili ya kubaini wahalifu, mihadarati, silaha na hata ufichuaji wa mabomu yaliyotegwa ardhini.

Kuna taarifa nyingi juu ya wanyama mbalimbali kutumika kutoa taarifa muhimu na hata kubashiri mambo fulani yanayotarajiwa kutokea. Wazee wa kijadi katika nchi walikuwa wanatumia mnyama fulani anayefanana na kenge (kaka kuona) ili kujua kama mwaka huo una masika au ukame. Wajerumani waliwahi kutumia pweza kubashiri matokeo ya kombe la dunia la kandanda. Haya ni machache tu katika mambo yanayoweza kuitwa lugha za wanyama.

Leo hii tuonapo maafisa wanyamapori wakiwa mahiri kujua tabia na mawasiliano ya wanyama isidhaniwe kuwa ni nguvu za giza bali ni elimu wanayojifunza vyuoni. Kwa vyovyote iwavyo elimu juu ya lugha ya ndege aliyofunzwa Nabii Suleiman, bila shaka kupitia ufunuo wa Allah ilikuwa ni muhimu mno kwa ajili ya maendeleo ya kijamii.

Uwepo wa mitandao ya habari inayojihusisha na elimu juu ya ndege na wanyama pori unathibitisha ukweli huu. Bila shaka dunia inayo deni kubwa kwa Nabii Suleiman ambaye yeye na baba yake waliitambulisha na kuiendeleza elimu hii duniani wakiacha urithi bora kabisa wa kielimu kwa vizazi vingi vilivyofuata. Hivyo ni wajibu wetu kuendeleza elimu hii na kuitumia kwa faida mbalimbali za jamii yetu hapo ndipo tutakuwa tumefikia ufahamu wa kweli wa maana ya 'MANTIQ AL TAIR' (Lugha ya ndege) elimu ambayo Allah Alimtunukia Hadhrat Suleiman (as).

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE





Sheikh Muhammad Munawwar Sahib

HABARI UK> 04


HAIBA YA MFALME SULEIMAN AS

Na Mwl. Abdullah H. Mbanga – Ikwiriri, Rufiji – Pwani.

Hadhrat Suleiman (as) ndiye Nabii anayetajwa kuwa maarufu Zaidi katika wana wa Israeli baada ya Musa (as). Suleiman pia anatajwa kuwa miongoni mwa wafalme wenye nguvu waliopata kutokea duniani.

Qur'an Tukufu inadokeza kwamba Suleiman alikuwa ni mtu aliyejaaliwa vipawa vingi vya hekima na utambuzi. (27:16). Kutokana na vipawa alivyojaliwa na pia umahiri na uadilifu aliouonyesha katika utawala wake, Suleiman (as) ameendelea kuenziwa sio na Waisrael tu, bali wanahistoria wengi wanamhesabu kuwa ni mtu wa kupigiwa m fano katika masuala ya utawala, uadilifu na ucha Mungu.

Kutokana na wema aliokuwa nao, Suleiman (as) alitokea kuwa mtu mwenye haiba kubwa katika zama zake.



Wafalme, wanazuoni na hata raia wa kawaida katika enzi hizo, walimhesabu Suleiman (as) kuwa ni m tu aliyekuwa

Zaidi ya binadamu wa kawaida. Katika kumuenzi Hadhrat Suleiman (as) riwaya nyingi

ziliandikwa juu ya sifa zake. Hekaya kuhusu vipawa na uhodari wa Suleiman katika medani mbalimbali ziliendelea

kuenezwa duniani kwa njia ya simulizi hata baada ya kifo chake.

Jambo la kusikitisha ni hili ya kwamba hekaya nyingi kumhusu Suleiman na maisha yake zilitiwa chumvi na wasimulizi – pengine kwa ajili ya kumpamba – hata ikapelekea kuibuka kwa taswira tofauti kabisa juu ya Suleiman na vipawa vyake. Pengine kutokana na ufahamu finyu juu ya baadhi ya aya za Qur'an Tukufu, hata baadhi ya wanazuoni wa Kiislam wamejikuta wakizikumbatia baadhi ya dhana potofu juu ya Suleiman na kuzihubiri kwa karne kadhaa katika vizimba vya Misikiti, Mikutano ya hadhara na hata kwenye madarasa mbalimbali. Hali hii ikapelekea Waislam wengi kuingiwa

HABARI UK> 11



Je, Wajua?

Kiichiro Toyota ndiye mwanzilishi wa kampuni ya Toyota Motor Corporation na Toyota group ya magari. Inamiliki kampuni tanzu nyingi, zikiwemo Daihatsu, Hino motors, Lexus.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 4,300/=.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com